BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Sita – Tarehe 19 Septemba, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

Wizara ya Afya:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Afya juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

58. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Mahabusu nyingi wanazohifadhiwa watuhumiwa katika vituo mbali mbali vya Polisi zimekuwa na hali mbaya na haziendani na muktadha wa mtazamo wa haki za binaadamu.

    Je, Serikali ina mkakati gani wa kuziboresha mahabusu hizi ili watuhumiwa waishi katika mazingira ya utu na ubinaadamu.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

28. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa jukumu la ukaguzi na udhibiti wa fedha za Serikali.

    Je, ni kwa kiasi gani jukumu la kudhibiti fedha limetekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

23. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Kumeibuka mijadala mbali mbali kuhusu ongezeko la Deni la Taifa, ingawa miongoni mwa sababu za ongezeko hilo ni kubadilika kwa kiwango cha ubadilishaji wa fedha (exchange rate).

    Je, ni kwa kiasi gani sababu hii imeathiri Deni la Taifa.

276. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na juhudi za Serikali, kiwango cha umasikini nchini kinazidi kuwa changamoto kubwa kwa maendeleo ya nchi. Umasikini umekuwa kikwazo kikubwa katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya kitaifa na umesababisha hali duni ya maisha kwa sehemu kubwa ya wananchi.

(a) Je, ni ipi tathmini ya kitaalamu juu ya asilimia ya wananchi wanaoishi chini ya mstari wa umasikini wa mahitaji ya msingi Zanzibar.

(b) Je, Serikali imewahi kufanya tathmini ya makadirio ya umaskini wa kipato kiwilaya kwa Zanzibar na tathmini hiyo iko vipi.

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu ya kupunguza kiwango cha umasikini na kuboresha hali ya maisha kwa wananchi wa Zanzibar.

<u>**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**</u>

107. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kipindi cha Safari kinachorushwa na TBC1 kimekuwa na ushawishi mkubwa sana wa kushajiisha utalii wa ndani kwa mafanikio makubwa.

(a) Kwa nini urushwaji wa vipindi vya vivutio vya utalii vilivyopo Zanzibar umekuwa mdogo mno kupitia ZBC.

(b) Ni lini ZBC itafikiria kuwa na kipindi mbadala kama cha Safari, katika kuona kwamba wananchi wanapata fursa ya kujionea wingi na utajiri wa vivutio vya utalii vilivyopo Zanzibar.

110. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tukiangalia rika la vijana wa kisasa tunapata mtazamo gani wa kujiridhisha kwamba mila, silka, hulka, desturi, mienendo na minenguo ya utamaduni wa Mzanzibari kwa ujumla unarithishwa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

8. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafas iza Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna tabia inayoendelea ya magari makubwa ya mizigo kupakia vitu vya hatari ikiwa ni pamoja na nondo, bila ya kuweka alama yoyote ya kutambulisha hatari hiyo.

(a) Kwa muda gani sasa Wizara yako imeligundua tatizo hili.

(b) Ni hatua zipi Wizara imezichukuwa katika kuliondoa kabisa tatizo hili.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

67. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, maboresho ya mtaala mpya (Competence Based Curriculum) unamuandaa vipi mwanafunzi wa ngazi ya maandalizi katika kuanza kujenga tafakuri na udadisi kabla ya kwenda ngazi ya msingi.

88. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Je, kwa kipindi gani kijacho Wizara yako itakuwa imeshafanya tathmini ya kwanza ya utekelezaji wa mtaala mpya wa kupima umahiri wa elimu nchini.

(b) Tutarajie kizazi cha aina gani katika kipindi hicho ikiwa kama ni mwanzo wa matokeo chanya ya mtaala huu mpya.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

96. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa kiasi gani Wizara yako inafuatilia kwa karibu zaidi vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vinavyofanyika na kuripotiwa katika skuli zetu.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

234. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Msitu wa Ngezi ni muhimu sana na kielelezo cha uchumi na maendeleo ya kijamii. Kwa bahati mbaya sana msitu huo kwa sasa umekabiliwa na changamoto tofauti ikiwemo ukataji wa miti, uhaba wa ulinzi na ufuatiliaji hafifu kwa wasimamizi wake.

Je, kwa kiasi gani Serikali inalitambua tatizo hilo na ina mkakati upi wa kuziondoa changamoto hizo.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

243. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali kwa kufanikisha mradi wa umeme kuweza kufika katika kijiji cha Kivumoni Mtambwe Kusini. Licha ya huduma hii kuanza kutumika, yapo malalamiko kutoka kwa wananchi ambao waliharibiwa vipando vyao na kuahidiwa na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kuwa watapata fidia, lakini mpaka sasa bado hawajapata fidia yoyote.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili la wananchi ambao bado wanasubiri fidia na ni lini wananchi hawa wategemee kulipwa fidia zao.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kutoa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya maendeleo kama hii.

(c) Kwa kuzingatia tathmini iliyowahi kufanywa na Wizara yako, je ni wananchi wangapi ambao wanadai fidia hizi kwa Zanzibar ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024 na ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha wanalipa fidia hizi ndani ya muda.

**Wizara ya Afya:**

50. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    (a) Tathmini iko vipi juu ya uelewa wa wananchi kwa ongezeko la maradhi ya homa hatari ya ini.

    (b) Ni kwa kiasi gani Wizara yako imeweza kuwafikia wananchi na kuwapa uelewa wa maradhi haya.

    (c) Anaathirika vipi mtu anaepatwa na ugonjwa wa maradhi ya homa ya ini.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

255. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

    Kumewahi kuripotiwa na wavuvi wetu wa ndani kuona meli kubwa za nje ya Tanzania zikifanya shughuli za uvuvi katika maeneo ya Zanzibar. Meli hizi zinasemekana huwa zinajishughulisha na uvuvi haramu kinyume na sheria za kimataifa.

    (a) Je, Serikali imewahi kuzikamata meli ngapi zilizoingia nchini bila ya kibali kwa kujishughulisha na uvuvi haramu.

    (b) Je, ni hatua zipi za kisheria huchukuliwa kwa meli hizi ambazo hukamatwa katika mipaka ya Zanzibar.

    (c) Je, ni leseni ngapi zimewahi kutolewa kwa meli za nje kuweza kufanya shughuli za uvuvi ndani ya mipaka ya Zanzibar na kiasi gani cha fedha kimepatikana tokea mwaka 2020 hadi leo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

71. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Kwa kuwa nchi ya Ureno ni moja kati ya nchi yenye mji unaohifadhiwa na UNESCO ambao unashabihiana sana kwa majengo na muonekano kama ulivyo Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Ni jambo gani linaloikwamisha Wizara yako kufanya mahusiano ya kirafiki kati ya miji hii miwili ya hifadhi kwa lengo la kuvuna watalii kutoka Ureno na kubadilishana uzoefu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Afya:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**19 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**